OFISI YA MWANASHERIA
MKUU WA SERIKALI

# WIKI HII MAGAZETINI NA MITANDAONI

24/03/2025 ► 29/03/2025

OAG

# Mawakili wa serikali wafundwa maslahi ya taifa

Na Matern Kayera, Arusha

MWANASHERIA Mkuu wa Serikali, Hamza Johari amesema ofisi yake imeweka mkakati wa kuwajengea umahiri mawakili wa serikali katika kushauri serikali vizuri kwa maslahi ya taifa, usalama wa taifa na uchumi endelevu katika sekta mbalimbali.

Johari alisema hayo wakati akifungua mafunzo ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa mawakili takriban 300 wa serikali wanaoshiriki mafunzo ya siku tano yaliyoandaliwa na ofisi yake jijini Arusha jana.

Alisema lengo la mafunzo wanayopata umuhimu mkubwa katika kuwajengea umahiri mawakili hao ili ushauri wanaoutoa usaidie serikali kufanya maamuzi sahihi bila kuingia katika migogoro na mtu au watu au taasisi nyingine.

"Lengo kubwa la mafunzo haya ni kukuza ubora wa kisheria kwa maendeleo endelevu. Tunataka ubora katika huduma za sheria uwe mzuri ili kuleta maendeleo kwa taifa letu, ndiyo maana tunawajengea umahiri. Sekta ya sheria ina mchango mkubwa katika maendeleo ya taifa katika sekta mbalimbali kama vile viwanda, biashara na nyinginezo," alisema Johari.

Aliongeza: "Hakuna kitakachofanyika bila kuwa na sheria mahususi iliyotungwa kwenye eneo husika au mikataba fulani ya kibiashara, ili kuwe na mikataba na miradi mikubwa, sekta zinazokua kiuchumi, lazima kuwe na sheria mahususi kwenye sekta mahususi kama kilimo, usafirishaji, SGR, Bwawa la Kufua Umeme la Julius Nyerere, biashara, nishati, madini na nyinginezo".

Hata hivyo, alisema Johari alisema kuna [illegible] mawakili wa kuhakikisha kufanya kazi zinazowapasa na kushauri hali inayoweza kuchangia Tanzania kufikia uchumi wa kati wa juu ifikapo mwaka 2050.

Alisema ubora katika huduma za sheria unataka mwanasheria kufanya kila jambo kwa wakati bila kuchelewa ikiwemo kufika eneo husika kwa wakati na kutoa huduma kwa wakati na kwa kuzingatia ubora.

"Imekuwa changamoto kwa nchi nyingi za Afrika na zinazoendelea watu kuwa goigoi katika utoaji huduma, hivyo kaulimbiu yetu ya weledi na ubora itakuwa ngumu kufikia kama hatutafanya kazi kwa haraka na kwa wakati. Usipofanya kazi kwa wakati unajizalishia [illegible] bila sababu ya msingi, na matokeo yake wateja wanakosa huduma," alisema Johari.

Aliongeza: "Huduma inapotolewa inakuwa na athari katika biashara, ukuaji wa uchumi; hivyo, pamoja na mafunzo haya kuongeza umahiri wetu katika sheria, pia tunataka kuona mfumo fikra wetu kwa kufanya kazi kwa haraka na ubora bila kuchelewa. Tunataka hilo tuliyone kama Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, kufanya kazi kwa haraka na kwa ubora".

Naye Mwandishi Mkuu wa Sheria, Onorius Njole aliwasisitiza mawakili hao katika maeneo mbalimbali ya kisheria ambayo wanapatiwa kuyazingatia katika kutoa ushauri sahihi kwa serikali bila kuwa [illegible].

Mwanasheria mstaafu, Sirilius Matupa aliwasisitiza mawakili hao kuzingatia weledi katika uandishi wa ushauri na uwasilishaji wa huo ushauri kwa wadau.

"Tumewasisitiza wawe mahiri kisheria, wajue tatizo wanalotolea ushauri, wauwasilishe kwa weledi kwa kutumia lugha rahisi inayoeleweka na wadau au mtu husika na wajitahidi kutotumia lugha ya [illegible], kwa kufanya hivyo, ushauri utamfikia mdau kama ulivyo na utamsaidia kutatua changamoto aliyonayo," alisema.

Mwandishi Mkuu wa Sheria Msaidizi-Idara ya Uandishi na Mratibu wa Mafunzo, Rehema Katuga alisema Mwanasheria Mkuu wa Serikali ana jukumu kubwa la kushauri serikali katika masuala ya kisheria ikiwemo mikataba, uandaaji, uandishi wa sheria, sheria mpya zinazotungwa na mambo mbalimbali yanayohusu shughuli za serikali.

Katuga alisema kupitia mafunzo hayo wanataka kuongeza umahiri kwa mawakili kusaidia changamoto ambazo serikali inapitia ikiwemo kuvunjwa kwa mikataba na mikataba kutosimamiwa vizuri ili kuongeza umahiri na tija kwa serikali.

# Capacity of state attorneys raised

From MATERN KAYERA in Arusha

THE Attorney General (AG), Mr Hamza Johari, has said that his office has developed a strategy to enhance the capacity of state attorneys, enabling them to better advise the government in the interests of the nation, national security, and sustainable development across various sectors.

Mr Johari made this statement while addressing approximately 300 state attorneys who are participating in a five-day training organised by his office in Arusha.

He said that the training is crucial for building the capacity of state attorneys so that the advice they provide helps the government make informed decisions.

"The main objective of this training is to promote legal excellence for sustainable development. We want the quality of legal services to be strong, as it plays a significant role in driving development across our nation. That's why we are focusing on enhancing their capabilities.

The legal sector has a vital contribution to the nation's development in industries such as trade, agriculture, transportation, energy and many others," said Mr Johari.

He continued, "Nothing can progress without specific laws or commercial agreements in place. For sectors such as agriculture, transportation, trade, energy and mining to thrive, there must be clearly defined laws and regulations governing them."

He stressed that quality legal services require state attorneys to perform their duties efficiently and on time, including arriving at relevant locations promptly and delivering services with the required quality.



oagtanzania
www.oag.go.tz



Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Samwel Maneno akizungumza na wanasheria na mawakili wa serikali wakati wa mafunzo ya kuwajengea uwezo na kuwakumbusha masuala ya kisheria kwa lengo la kuboresha utendaji kazi jijini Arusha jana. (Picha na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu).

## Mawakili wa Serikali wapewa mafunzo

Na Mwandishi Wetu

OFISI ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali inaongoza mafunzo ya siku 5 ya Mawakili wa Serikali jijini Arusha kwa lengo la kuwajengea uwezo, ubobevu na umahiri wa utekelezaji wa majukumu yao Mawakili wa Serikali.

Mafunzo hayo ya pili ya Mwaka mahsusi kwa ajili ya Mawakili wa Serikali ( Bespoke Training for State Attorneys 2025) yanayofanyika jijini Arusha kwa siku tano kuanzia Machi 24 hadi 28, yamehusisha Wakurugenzi wa Idara za Sheria za Taasisi Mbalimbali ,Wakuu wa Vitengo vya Sheria na Maafisa Sheria

na yana lengo la kuwaongezea uwezo Mawakili wa Serikali, ubobevu na Umahiri katika Utekelezaji wa majukumu yao na kuisaidia serikali katika maeneo ya kisheria yenye changamoto.

Awali, akimwakilisha kwa niaba ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Mkurugenzi wa Uratibu na Huduma za Ushauri wa Kisheria Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali Neema Ringo alisema, mafunzo hayo ni muhimu kwa mawakili hao wa Serikali kwani wamekuwa kiungo muhimu kupitia taasisi zao kwa kutoa ushauri wa kisheria kwa serikali na Wizara zao.

Aliongeza kuwa lengo la Mafunzo hayo, ni kuongeza umahiri, ubobevu katika maeneo mbalimbali hususani maeneo ya Mikataba yenye maslahi mapana kwa nchi hasa kwa kipindi hiki ambacho Serikali inatekeleza miradi mingi ya kimkakati kuelekea Dira ya Taifa ya 2050.

Aidha,katika mafunzo hayo mawakili hao wa Serikali watakumbushwa wajibu wao wa kulinda maslahi ya Taifa Mikataba ya kitaifa na kimataifa, pamoja na kulinda na kukuza Uwekezaji, Uendeshaji wa Sheria, Ununuzi na masoko ya kimataifa, majadiliano na usimamizi wa mikataba inayoingiwa na Serikali na kuboresha maeneo mbalimbali ya kisheria kwa kuongeza umahiri wa kada hiyo muhimu kwa maslahi mapana ya nchi.

6 UCHAMBUZI

TAHARIRI

HabariLEO

## Mafunzo haya kwa mawakili wa serikali yawe endelevu

KWA siku tano kuanzia jana jijini Arusha, mawakili wa serikali takribani 300 wanafundwa mambo mbalimbali, ikiwamo kuzingatia maslahi ya taifa wanapotekeleza majukumu yao katika kuishauri vizuri serikali kwenye eneo hilo la sheria.

Kwa mujibu wa Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Hamza Johari, ofisi yake imeweka mkakati wa kuwajengea umahiri mawakili wa serikali katika kuishauri serikali vizuri kwa maslahi ya taifa, usalama wa taifa na uchumi endelevu katika sekta mbalimbali.

Kama ambavyo majukumu ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali yamefafanuliwa katika Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ofisi hii ina umuhimu mkubwa katika kuimarisha na kujenga mustakabali wa nchi.

Sheria ni eneo mojawapo ambalo ni nyeti na kwa unyeti wake huo ina maana ni muhimu kwa wasimamizi wote wa sheria, wakiwamo mawakili wa serikali kutambua dhima na majukumu waliyobeba kwa niaba ya Watanzania wenzao.

Kwa maingi hao, kila jambo wanalolitenda ni lazima lizingatie maslahi makubwa ya taifa, usalama wa taifa na kubwa jingine, eneo la kiuchumi ili kuiwezesha nchi kupiga hatua za kimaendeleo bila kuwa na mikwamo ya kisheria.

Tunafahamu kuwa, Rais Samia Suluhu Hassan amefungua nchi na kuvutia sana uwekezaji nchini, hivyo kuna mikataba mingi ambayo serikali inaingia na taasisi na kampuni za nje zinazokuja kuwekeza nchini.

Hili ni eneo mojawapo ambalo ushauri wa mawakili wa serikali na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali wanapaswa kuwa na weledi nao ili serikali isijikute inaingia katika migogoro na wawekezaji nchini.

Hivyo tunafarijika kuona kwamba Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali imeona umuhimu wa kuwanoa mawakili wa serikali katika mambo haya mazito ili wanapofanya majukumu yao wawe na weledi mkubwa na waishauri vizuri serikali katika masuala yote yenye maslahi kwa nchi.

Sisi tunaamini mafunzo haya yana mchango mkubwa katika kuboresha na kustawisha masuala mbalimbali nchini na hasa mchango katika uchumi, kwa sababu ya kuwapo kwa miradi mingi ambayo kimsingi ina mikataba ambayo inapaswa kuwa imetengenezwa kwa weledi na inaakisi kile serikali inachokilenga.

Tunaishauri Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali iendelee kutoa mafunzo haya ya mara kwa mara kwa mawakili wa serikali ili kuwaongezea maarifa katika utendaji wao wa kazi na hivyo mchango wao katika ujenzi wa taifa kiuchumi utakuwa mkubwa.

Hii itasaidia sana kutokana na ukweli kuwa sheria zinaanzia kutungwa kwao, lakini pia ndio washauri wakuu wa serikali katika masuala ya kisheria na kimsingi ndio msingi wa mambo yote yanayofanyika katika taifa.

This Space can Only be yours
Call us today on +255 754 271 266



# MWANASHERIA MKUU ATOA WITO KWA MAWAKILI WA SERIKALI: “TUFANYE KAZI KWA HARAKA NA UBORA”

MICHUZI BLOG AT TUESDAY, MARCH 25, 2025 HABARI,

Na Pamela Mollel, Arusha

**Arusha, Machi 25, 2025** — Mwanasheria Mkuu wa Serikali, *Hamza Said Johari*, ametoa wito maalum kwa Mawakili na Wanasheria wote wa Serikali kuzingatia ubora na weledi katika utoaji wa huduma za kisheria, huku akisisitiza umuhimu wa kufanya kazi kwa wakati ili kuchochea maendeleo ya Taifa.

Akizungumza jijini Arusha katika mafunzo ya pili ya mwaka kwa Mawakili wa Serikali, Mhe. Johari alieleza kuwa ucheleweshaji usio wa lazima katika utoaji wa huduma umekuwa ni changamoto kubwa kwa nchi nyingi za Afrika, na Tanzania haiwezi kukwepa kuathirika endapo haitachukua hatua madhubuti.



BONGO5 | HABARI | BURUDANI | MICHEZO | VIDEOS | Log in

# Mawakili wa Serikali wakumbushwa majukumu yao katika kutoa ushauri wa kisheria

Yasini Ngitu · 15 hours ago · 1 minute read

Facebook | X




TBC Digital
YA RAIS SAMIA
UPDATES
Mwanasheria Mkuu ataka weledi kwa mawakili
TBC Digital | Tangaza Nasi Hapa
@tbc_online
//www.tbc.go.tz

oagtanzania



View insights | Boost post

35 | 1

Liked by **wilymcharlie** and others

**oagtanzania** HABARI PICHA

Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Mhe. Samweli M. Maneno amehudhuria kikao cha Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria kilichofanyika tarehe 24 Machi, 2025 Bungeni Jijini, Dodoma.

oagtanzania




View insights

Boost post

oagtanzania




View insights

Boost post

33 3

Liked by **ipyanamlilo** and others

**oagtanzania** Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali inaongoza Mafunzo ya siku 5 ya Mawakili wa Serikali jijini Arusha kwa lengo la kuwajengea uwezo, ubobevu na umahiri wa utekelezaji wa majukumu yao Mawakili wa Serikali.

# MITANDAONI

**oagtanzania**
Edited · 3d




View insights | Boost post

24

Liked by **ipyanamlilo** and others

**oagtanzania** Colonel Joseph Simbakalia akitoa mada kuhusu 'Jukumu la Mawakili wa Serikali katika Kukuza Uzalendo, Kulinda Maslahi ya Taifa, na Kuwezesha Usalama wa Taifa.'

#suluhuyaumahiri

**oagtanzania**




**oagtanzania**



OFISI YA MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI TANZANIA
WELEDI NA UBORA
PROFESSIONALISM & EXCELLENCE
THE OFFICE OF THE ATTORNEY GENERAL TANZANIA

# TUPO KARIBU YAKO!

## Tufuatilie kupitia

oagtanzania

info@oag.go.tz

www.oag.go.tz

Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali
Mtaa wa Mtumishi
Mji wa Serikali Mtumba
S. L. P 630
Dodoma - Tanzania

**KWA MSAADA WA HUDUMA ZA KISHERIA PIGA SIMU BURE 0800 11 0188**

Weledi na Ubora